# Yale Maungamo Mazuri

*1Timotheo 6:12; "Piga vita vile vizuri vya Imani; shika uzima ule wa milele ulioitiwa,*

*ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi".*

Tunataka tuangalie, kile Nabii wa Mungu wa saa hii amesema juu ya hilo:

Sasa, kumbuka, kila baraka ya ukombozi tayari imekwisha nunuliwa (lipwa). Gharama imelipwa. Na kuna njia moja tu ambayo unaweza kuipokea, ni kuiamini na kuikubali hiyo. Yeye ni kuhani mkuu wa maungamo yetu (Waebr. 4:14-16; 3:1-6). Ile barua kwa Waebrania inasema "Yeye ni kuhani mkuu wa maungamo yetu". Kukiri na kuungama ni jambo lile lile hasa. Yeye ni kuhani mkuu wa maungamo yetu. Kwa hiyo, Hawezi akatufanyia jambo lolote mpaka kwanza tumelikiri kwamba yeye amelifanya. Na sasa tunapoliungama hilo, hapo sasa Yeye ni kuhani mkuu, mwombezi/mpatanishi anaingia kazini kulishughulikia na kulifanya liwe sahihi. Kwa hiyo tunaomba, tukimtegemea Mungu usiku wa leo, katika ukarimu wake na huruma, kwamba Atatupa kwa wingi wa neema usiku wa leo. Na sasa kumbuka ni lazima ulikubali.

Mwenye dhambi anaweza akaja hapa madhabahuni kama kijana mwanaume au mwanamke katika umri wa miaka kumi na nne, na watakuletea wewe chakula chako hapa na ungemlilia Bwana hata uwe na umri wa miaka tisini, bado hutaokolewa hata kidogo. Ni lazima kwanza ukubali yale aliyokufanyia wewe. Unaona? Ni lazima ulikubali hilo wewe mwenyewe. Sasa unapolikubali hapo sasa Yeye ni Kuhani Mkuu, Mpatanishi/mwombezi kufanya maombezi juu ya maungamo yako ya kile unachoamini.
Kwa hiyo hawezi kufanya chochote mpaka kwanza tumekiri kwamba Yeye amelifanya. Unaona, uje hapa madhabahuni na uombe usiku kucha, haitakufanyia jambo lolote zuri mpaka uamini kwamba Yeye amekusamehe wewe, hapo unasimama juu. Sasa kwa kadiri ya Imani uliyonayo, hapo ndipo uli ……….. ulipoishi wakati ulipokuwa chini hapa katika tope la dhambi. Sasa, ninyi mliookoka karibuni, sasa mmeamini mmeokolewa si ndiyo? Hivyo uliinuliwa juu hapa, umeinuliwa juu kidogo, nini inafanya hiyo? Ni imani yako, kwa sababu unaamini ya kuwa wewe sasa ni mkristo; utaishi juu ya jambo hilo sasa unaona? Sasa kama unapenda kuinuka juu kidogo, kuwa na imani nyingi zaidi kwa sababu haina kikomo uendelee tu.

Vema oh lisilowezekana linaweza kufanywa kuwa halisi. Mambo yote yanawezekana kwao waaminio (Marko 11:22 – 24). Hiyo ni kweli" Kama ukiuambia mlima huu, ng'oka na usione shaka moyoni mwako, unaamini ulilonena litatokea basi unaweza kupata kile ulichonena".

Sasa angalia hawa sabini, walirejea nyuma kwa sababu hawakukubaliana naye kwa lile walilofikiri ni sahihi (Yoh. 6:60-66), Luka 10:17-20). Hatuna wazo la kuwazia ni kile Yeye alichokisema. Kataa kule kuwazia kwako. Wewe sema tu kile alichokisema. Hayo ndiyo maungamo halisi. Maungamo maana yake ni kusema jambo lile lile.

Kama nitakiri kwamba jambo fulani limetendeka ninasema jambo lile ambalo limetendeka. Hayo ndiyo maungamo halisi yalivyo; naye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu. Kusema jambo lile lile Mungu alilosema, unaona, hiyo inalifanya hilo kuwa sahihi kwa sababu unarudia tu Neno la Mungu.

Hutumii mawazo yako; unatumia mawazo Yake. Iweni na nia ile ile ndani yenu nia iliyokuwa ndani ya Kristo (Filipi 2:1-11) unaona? Fikiria anavyofikiria Yeye. Sema anavyosema Yeye. "Kuungama" ni "Kusema jambo lile lile". Kuungama ni kuungama jambo lile lile. Kusema jambo lile lile. Sasa usikiri mawazo ya akili zako, zaliwa mara ya pili na ukiri Neno Lake. Ungama alichosema, huko ndiko kukiri. Sema "Kwa kupigwa

kwake sisi tuliponywa”. (Isaya 53:4-5) kwa kupigwa kwake, nina haki kwa majeraha yake, sasa hivi, nina haki ya wokovu. Nina haki ya Roho Mtakatifu. Aliniahidi hilo. Akisema ni kwa ajili yenu na watoto wenu, na kwa wote walio mbali na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie (Matendo 2:37-41). Naamini hilo kwa vizazi vyote.

Nashangaa juu ya watu wale. Nilikutana nao kwenye huduma ya uponyaji. Nimeona watu wakija mimbarani, wakiwa ni vipofu kabisa. Na kuja na kuchukua ……… Baada ya kuombewa na kuponywa na kusoma Biblia, wakitembea pale na kumsifu Mungu. Na kukutana nao baada ya miezi sita na wamekuwa ni vipofu kama walivyokuwa mara ya kwanza.

Sasa, hapana, uponyaji una nguvu kama imani yako ilivyo na utadumu kwa kadiri ya imani yako.

Inategemea imani yako inasimamia wapi. Wokovu wako ni mzuri ili mradi maungamo yako ni mazuri. Lakini maungamo yako yanapoanguka, hivyo na wokovu wako umekwenda. Kwa maana Yeye ni Kuhani Mkuu aliyeketi mkono wa kuume wa Mungu kufanya upatanisho kwa maungamo yako, hicho ndicho kinachotokea.

Sasa, uone hapa ni kitu gani, marafiki, unaona, kama unalipata, wewe ni mkristo kwa sababu unaamini wewe ni Mkristo. Na hayo yako sawa kwa sababu Yeye ni Kuhani Mkuu.

Sasa, angalia, Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu. Unapata ninachomaanisha? Kile unachokiri ndicho ulicho. Mtu yeyote hataweza kamwe kuishi zaidi au juu ya kile anachoamini .

Mchukue mtu anayezungumza juu ya kunywa wakati wote. Yeye anazungumza kunywa; Anafikiri juu ya kunywa; ataangukia chini kwenye kundi hilo na kuwa mlevi. Mtu anayefikiria juu ya mambo machafu, anaangalia mambo machafu; Anafikiri vitu vichafu, anasoma juu ya uchafu ………….

Huwezi kuishi juu ya kile unacho kiri kuwa uko. Ni kukiri kwako kunakokuokoa wewe.

Yeye anayenikiri mbele za watu, Nitamkiri mbele za Baba na malaika watakatifu (Matayo 10:32-33) Unaposema unaumwa, unaumwa. Sasa siyo ninahubiri ukristo wa kisayansi. Ninahubiri nguvu za Mungu. Na Roho Mtakatifu anashuhudia hilo, unaona?

Angalia sasa ilivyo. Unamkubali Yeye kwa kuwa unajisikia kwamba Amekuokoa wewe. Na unaenda ukiwaambia watu, ukishuhudia hilo na kuamini ushuhuda wako, na utatenda haki. Itafanya jambo hilo hilo kwa uponyaji.

Yeye siyo tu ni Neno, lakini ni Kuhani Mkuu wa Neno Lake Mwenyewe, tutalioneaje shaka hilo? Itawezekanaje tumwendee Yeye na tuache kuamini kwamba tunapokea tunachomuomba? Yeye ni Neno na ni mtetezi wa NENO. Yule Logosi akawa Neno Yohana 1:1-3, 14) na Neno akafanyika Mwili, na mwili huo ulikuwa Neno, ukapokelewa juu utukufuni, na sasa Yeye ni Kuhani Mkuu akifanya utetezi kwa Nafsi yake kulihusu Neno lake.

Sasa kumbuka, siyo vile umelia sana; siyo vile umetubu; siyo vile unavyoweza kumlilia Mungu kwa sauti kuu; siyo vile unavyojaribu kuwa muaminifu; ni kwa kiasi cha imani yako uliyonayo pale unapomwendea Yeye. Hakuokoi kwa ustahivu wa maombi yako. Hakuokoi kwa ustahivu wa haki yako. Anakuokoa kwa ustahivu wa Imani yako. Ni kwa imani unaokolewa na ni kwa njia ya Neema (Efeso 2:8-9).

Sasa, unakuja mimbarani ukitambua kwamba u mwenye dhambi na unasikitika kwa dhambi zako. Unatubu juu ya yale uliyoyafanya. Na unaweza ukakaa hapo na ulie mwanzo wa wiki hata mwishoni, na haitaweza kamwe kukuokoa mpaka uamini moyoni mwako kwamba umeokolewa. Hiyo ni kweli? Hapo unakiri hilo.

Sasa, Hawezi akakufanyia mpaka umelikiri hilo. Hiyo ni kweli? Kwa maana Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo. Hawezi kufanya lolote ……….” Ukinikiri mimi mbele za watu, nitakukiri wewe mbele za Baba”. Hayo ni kweli? Kile unachosema nimekutendea hapa chini, Ndivyo nitakavyomwambia Baba kwamba …………..

Hayo ndiyo niliyokutendea wewe". Yeye ni Kuhani Mkuu. Unalipata hilo kijana mdogo? Kuhani Mkuu wa maungamo yako.

Sasa, Yeye amekaa hapa kufanya utetezi kwa ajili ya maungamo yangu, na ninayo haki ya kukiri kwamba Yeye amefanya kila kitu kilicho kwenye baraka za ukombozi kwa ajili yangu. Angalia hilo.

Baraka za ukombozi ilikuwa ni nini? Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. (1Petro 2:24). Hiyo ni kweli? Hiyo ni miliki ya kila mwaminio. Hiyo ni yangu.

Basi ungama, nini? Kwa kupigwa kwake sisi tumeponywa; Kwa neema Yake nimeokolewa. Kwa ahadi Yake, nitatii, na nitajazwa na Roho Mtakatifu" (Matendo 5:32) Angalia hilo. Kama umeshawishika kwamba anatimiza Neno lake, lakini kwanza yapasa ushawishike. Na silaha zote za Mungu ni za kimbinguni. Silaha za Mungu ni nini; Upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, upole, fadhili, subira, imani (Galatia 5:22-23) kwa hiyo mambo yote ya kiasili yanafanyika kama sadaka kwa Kristo. Sisi tunaamini tu. Ni kwa Imani. Hakuna cha kuona, hakuna cha kujisikia. Inakupasa uliamini. Yesu hata wakati mmoja hajawahi kusema, "Je umeiona" Je umejisikia, yeye alisema Je mnaamini hilo? ……… Je uliamini hilo?

Itafaa nini ndugu zangu, hata mtu aseme anayo imani na hana matendo? Je imani yaweza kumuokoa (Yakobo 2:14) haiwezekani kama umeamini Mungu atakuokoa, inabidi uliamini na kisha uungame kwamba Yeye amekwisha kulitenda, kabla halijatendeka ………… Na inatenda kazi kuwa ni haki.

## Nukuu za Kiingereza

Kumwita Yesu kwenye kituko (64-0319), Aya 5-6, 168; ujumbe wa neema Aya 177

Waamini wa aina tatu uk.22; KRISTO(55-0221) Aya 49, Maisha yaliyofichika na Kristo (56-0213) Aya 20-23, Huduma inaelezewa (50-0711) Aya 55, Je unaamini Hili?

(50-0716) aya 11 Mkuu na mshindi mwenye uwezo (57-0421 M) Aya 27, udhihirisho wa roho (51 – 0717) Aya 19 Kuhusika na kushawishika (62-0610E)Uk.27, Mungu hutimiza Neno lake (57-0307 Aya 57). Agizo langu (51-0505)Aya 35

Jiwe la kujengea la kiroho no. 138 kutoka kwenye Neno lilofunuliwa la saa hii imekusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr.69, D-75328 Schomberge Germany

Phone(+49) 72357613, Fax (+49)72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao utakuwa ni Biblia moja kwa moja na kazi ya haraka itaizunguka dunia. Mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu ya Mungu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

Ndugu Branham katika Mwenendo na utaratibu wa mafundisho uk. 724.

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E.Y. Kanju*
*Box 553 Korogwe Tanga*
*E-mail: chaelika@livel.com*
*cellphone: 0713230098/0684230098*